**TALKING NOTE ZA MHE. THOBIAS ANDENGENYE MKUU WA MKOA WA KIGOMA WAKATI WA KUZUNUMZA NA WANANCHI WA MNANILA ENEO LA ONE STOP CENTRE KUHUSIANA NA UTUNZANIA NA KULINDA MAZINGIRA**

**TAREHE 29 OKTOBA 2021**

**==================**

**Ngd. Rashi Kassim Mchatta-Katibu Tawala wa Mkoa**

**Mhe. Ester Mahawe Mkuu wa Wilaya ya Kgoma,**

**Mhe. Col. Masala Justine Ngayalina- Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe,**

**Mhe. Hanafi Msabaha –Mkuu wa Wilaya ya Uvinza**

**Mhe. Jackson Mateso-Mwenyekiti wa Halamshauri ya Uvinza**

**Mhe. Venance Sylvester Kigwinya - Mwenyekiti wa Halmashauri,**

**Ndg. Lukindo Hiza -Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la TUUNGANE na Maafisa.**

**Watendaji kutoka Sekretarieti ya Mkoa,**

**Wakurugenzi wa Halmashauri za Uvinza na Buhigwe,**

**Makatibu Tawala wa Wilaya ya Uvinza, na Buhigwe**

**Wataalam mbalimbali wa Idara ya Maliasili,**

**Wananchi na**

**Waandishi wa Habari,**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sote afya njema na kutuwezesha kukutana hapa. Pia, niwashukuru Wananchi kwa kujitokeza katika mkutano huu. Ama baada ya salam na shukrani hizo ninaomba niwaletee Salam nyingi kutoka kwa Viongozi wetu wa Nchi.

Kwanza nawaletea Salam kutoka kwa Mhe. Samia Suluhu Hassa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasema anawapenda sana na yupo pamoja na sisi wote wana Buhigwe na Kigoma kwa ujumla.

Pili, nawaletea Salam kutoka kwa mpendwa wetu, ndugu yetu kaka yetu Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawasalimu sana na anasema tuendelee kuchapa kazi kuinga mkano Serikali ya awamu ya sita ili kazi iendelee kwelikweli.

Tatu, nawaletea Salamu kutoka kwa kiongozi wetu Kasssim Majali Majaliwa (Mb), Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawapongeza kwa kuendeleaa kuingua mkono Serikali ya awamu ya sita anawapenda sana wananchi wa Buhigwe.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Aidha, baada ya salamu hizo kutoka kwa viongozi wetu wapendwa naomba nizungumzie jambo ambalo limetuleta katika eneo hili la Manyouvu.

Tumekuja kukagu na kuangalia eneo hili ambalo kimsingi ndipo kilipo chanzo cha mto Malagarasi. Mto Malagarasi huu ni muhimu sana katika mkoa wetu na Taifa, kwani ndio uonapeleka maji katika ziwa Tanganyika ambalo kwa namna moja ama nyingine linatupatia chakula, linatuletea mvua, na kutoa ajira kwa Wananchi. Tusipolinda chanzo cha maji ya mto Malagarasi tunaweza kukosa vyote hivi. Eneo hili ambalo ni chanzo cha mto linapaswa kulindwa, kutunzwa na kuendelezwa kwa kupanda miti rafiki, na kuhakikisha hakuna shughuli za kibinadamu zinazofanyika katika eneo hili.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Nawahimiza sana kutunza vyanzo vya maji Sheria ya Mazingira inaeleza kutokufanya shughuli zozote katika maeneo ya vyanzo vya maji kwa umbali wa mita 60, tunapaswa kuzingatia hilo kuepuka kuendesha shughuli za kibinadamu maeneo ya vyanzo vya maji kama vile kulima, kukata miti na shughuli nyinginezo ambazo zihatarusha uoto wa asili katika vyanzo vya maji.

Kuhimiza upandaji miti

Nawahimiza tuwe na tabia ya kupanda miti mingi katika maeneo yetu, nyumbani kwenye taasisi na katika maeneo ya wazi, miti ni muhimu sana katika kutunza mazingira lakini pia kupendezesha mazingira yetu.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,**

Shughuli mbalimbali za kibinadamu zimekuwa tishio la uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji, mapori ya akiba, na hifadhi za taifa katika Mkoa wetu.

Kwenye maeneo mengi tunashuhudia mapori, vyanzo vya maji na hifadhi zikivamiwa na kutoweka. Wananchi tunalo jukumu kubwa la kushirikiana na Serikali pamoja na Wataalam kulinza mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

Juzi nimezindua program ya upandaji wa miti Milioni Moja na Sitini Elfu (**1,060,000**) yenye thamani ya Shilingi Milioni Mianne laki tatu na Sabini na Nane Elfu (**446,315,788/=)** iliyogharimiwa na Shirika la TUUNGANE kwa kuona umuhimu wa kushirikiana na Seriakli katika kulinda mazingira na rasilimali.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Miche hiyo itagawawiwa katika maeneo mbalimbali, Wananchi na wadau mbalimbali tunalo jukumu kubwa la kutunza mazingira na kulinda mapori na misitu katika maeneo yetu na kuhimiza upandaji wa miti. Tusipodhibiti tabia za uharibifu wa Mazingira kama vile kuchoma moto miti tunaua misitu ya asili na kutengeneza jangwa ambapo athari zake tusipoziona leo basi kesho vizazi vitaathirika kwa ukame na mabadiriko ya tabia ya nchi.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Aidha, kabla kuhitimisha hotuba yangu naomba niwakumbushe mambo mawili la kwanza muendelee kuchukua tahadhari ya janga la UVIKO 19 kwa kufuata maelekezo ya Wataalamu wetu wa Afya ikiwemo kuendelea kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuvaa barakoa, kuepuka misongamano isiyo ya lazima na pia Kutumia fursa ya kuchanja kwani kuchanja ni kujiweka salama zaidi ya maambukizi na utakapougua usiwe katika hali tete ya kuwekewa Mitungi ya gesi na kukaa muda mrefu hospitalini.

Pili, nchi yetu inatarajia kuwa na zoezi la Sensa Mwaka 2022 kwa mwezi ambao Serikali itatangaza, niwaombe Wananchi wote washiriki katika zoezi la kuhesabiwa ili kuwezesha nchi kutengeneza mipango na Sera zinazoendana na Idadi ya Wananchi waliopo, zoezi la Sensa ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi na kwa kila Mwananchi, hivyo wakati ukifika wa kuhesabiwa Wananchi wote watoe ushirikiano kwa wataalamu watakaofika kwenye maeneo kuwahesabu

**Asanteni Sana Kwa kunisikiliza**

**=======================================**